## Kusoma Zaidi

# Mbinu za kufundishia msamiati.

### a) Mbinu ya kutumia maelezo

Kuna maneno ambayo kuelezeka maana yake hujitokeza bila utata. Mbinu hii inaweza kutumiwa kueleza baadhi ya maneno. Hata hivyo, yapo maneno ambayo kueleza maana yake huwa na utata. mbinu mbadala hutumiwa katika hali hii. Kwa mfano; neno kalamu, ukitoa maelezo yake yanaweza kueleweka kwa wepesi. maelezo ya neno kalamu yaweza kuwa; kalamu ni kifaa kinachotumiwa kwa kuandika. Inaweza kutumia wino ya kuongezwa mara kwa mara au inaweza kuwa ile iliyowekwa kutumika hadi wino uishe.

### b) Mbinu ya kutumia picha

Maana ya neno inaweza kutolewa kwa kutumia picha hasa kwa maneno ambayo yanaweza kuwa na utata. Maneno, kiboko, buibui na beberu miongoni mwa mengine maan yao inaweza kutolewa kwa kutumia mbinu hii. matumizi ya picha kutoa maana ya maneno haya yanaweza kutoa maana inayoweza kueleweka kikamilifu.

| | | |
|---|---|---|
|  Kiboko |  **Beberu** |  Buibui |

## Kusoma Zaidi

**c) Mbinu ya kuigiza au kuonyesha matendo kuhusu neno**

Kuna maneno ambayo yanaweza kutoa maana yake kikamilifu kupitia matumizi ya mbinu ya maigizo.
Kwa mfano maneno;



Kucheka,



Kula,



Kuamkuana,



Kuogelea.

## Kusoma Zaidi

**d) Mbinu ya kutumia kisawe**

Maneno yaliyo na visawe yanaweza kutumiwa kutoa maana ya msamiati kama mbinu ya kufundishia. Neno linaloeleweka kimaana, linasaidia kutoa maana ya neno ambalo linachukuliwa kama msamiati.

**Kwa mfano;**

a) **Ghulamu** - Mvulana

b) **Banati** - Msichana

c) **Darahimu** - Pesa

**e) Kutunga sentensi kwa kutumia neno**

Ufananuzi wa msamiati unaweza kufanywa katika matumizi ya neno kwenye muktadha wa sentensi. Maana ya neno inaweza kuwa wazi inapotumiwa katika sentensi. Maneno yenye utata yakitumiwa katika muktadha wa sentensi yanaweza kueleweka na hasa kupitia upatanisho wa kisarufi. Kwa mfano;

a) **Kiboko a**liyejifungua alipatikana majini asubuhi.

b) Nilifanya kazi **barabara.**

Kumbuka kwamba mbinu zinaweza kutumiwa kimwingiliano ili kutoa maana ya msamiati kikamilifu. Mwalimu anaweza kutumia moja au zaidi katika mchakato wa kufundisha. Kutambua maana ya msamiati kunasaidia kusoma na kufahamu ujumbe kwenye ufahamu kikamilifu.